

## Mchango wa Mbinu ya Familia Wenyiji katika Ufundishaji na Ujifunzaji Darasani wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni

*Said Omari Said  
MS Training Centre for Development Cooperation (MS TCDC)*

### Ikisiri

Familia Wenyiji ni moja kati ya mbinu mashuhuri zinazotumika katika ufundishaji wa lugha za kigeni kwa kuzingatia ufundishaji kimawasiliano. Tafiti mbalimbali zimeonesha umuhimu na ufaafu wa mbinu hii katika maendeleo ya ujifunzaji lugha kwa wajifunzaji wa lugha ya kigeni. Licha ya kuwepo uhusiano kati ya mbinu hii na ufundishaji na ujifunzaji wa lugha darasani, tafiti hizo hazikuonesha mchango wa matumizi ya mbinu hiyo katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni darasani. Makala hii imebainisha mchango wa mbinu hiyo katika ufundishaji na ujifunzaji wa darasani wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa kuchunguza ni kwa namna gani walimu na wajifunzaji wanatumia familia wenyiji kama mbinu ya kufanikisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa darasani. Data za makala hii zimetokana na mahojiano yaliyofanyika kwa kuhusisha walimu wa Kiswahili kwa wageni, wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni na waratibu wa familia wenyiji kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Chuo cha Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa (MS TCDC) na kuchambuliwa kwa mkabala wa kimaelezo na kuongozwa na Nadharia ya Umahiri wa Kimawasiliano na Tamaduni Mchanganyiko ya Hall (1992). Matokeo ya utafiti yaliyojadiliwa katika makala hii yameonesha upo mchango wa matumizi ya mbinu hii katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni darasani.

**Maneno Muhimu:** Mbinu, Familia, Wenyiji, Ujifunzaji, Ufundishaji.

### Utangulizi

Ufundishaji wa lugha ya kigeni umepitia mabadiliko mbalimbali ya kimikabala (Richards na Rodgers, 1986). Kuanzia karne ya 20, msisitizo uliwekwa zaidi katika mkabala wa kimawasiliano amba huzingatia zaidi umahiri wa kimawasiliano kuliko umahiri wa kisaruffi (Richards na Rodgers, 1986 na Larsen-Freeman, 2000). Ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni (kuanzia sasa LK) kwa kuzingatia mkabala wa mawasiliano huweza kufanyika kwa kutumia mbinu mbalimbali. Mojawapo ya mbinu za ujifunzaji wa LK ni kuchangamana na wazawa wa lugha husika ili kufikia kiwango cha juu cha umilisi (Macheno, 2008 na Wong, 2015). Wajifunzaji wa lugha za kigeni huenda katika nchi zinazozungumza lugha wanazojifunza kuititia programu mbalimbali kwa lengo la kupata fursa ya kujifunza kindakindaki lugha na utamaduni unaohusika (Wong, 2015). Programu hizi ambazo hupeleka wajifunzaji katika nchi mbalimbali hufahamika kama programu za ujifunzaji lugha ng'ambo<sup>1</sup>. Katika programu hizi, wajifunzaji hupewa fursa ya kuishi ama na familia wenyiji, hotelini, mabwenini au katika makazi ya kupanga mitaani.

Wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kutoka nchi mbalimbali huja nchini Tanzania kuititia programu mbalimbali za ujifunzaji lugha ng'ambo. Programu hizi huandaliwa na ama vyuo wanavyotoka wajifunzaji au serikali za nchi zao. Lengo kuu ni kuwasaidia wajifunzaji kupata fursa ya kufika nchini Tanzania kwa ajili ya kujiendezea na Kiswahili katika muktadha halisi. Kuititia programu hizi,

---

<sup>1</sup> Tafsiri ya 'Language Study Abroad Programs'

wajifunzaji hupelekwa kukaa na familia wenyeji<sup>2</sup>. Familia hizi hutumika kama mbinu ya kufundishia na kujifunzia Kiswahili kwa wajifunzaji hawa ambao wamepata fursa ya kushiriki katika programu hizi za kujifunza LK ng'ambo. Mbinu hii ya kukaa na familia wenyeji hutolewa kwa lengo la kuwapatia wajifunzaji muda mrefu wa kufanya mazoezi ya kile ambacho wanajifunza darasani katika familia ambako lugha wanayojifunza inatumika zaidi na ni katika muktadha halisi.

Tafiti nyingi za awali zimeonesha mchango wa matumizi ya mbinu hii katika ujifunzaji LK. Tafiti hizi zimebainisha mchango wa mbinu hii katika ujifunzaji LK ni kama vile kukuza kiwango cha umilisi wa lugha, kupata fursa ya kutumia lugha katika mazingira halisi, kufanya mazoezi ya lugha na familia kwa muda mwangi na kujifunza utamaduni wa lugha husika (Isabelli, 2000; Macheno, 2008; Parry, 2014; Di Silvio, Donovan na Malone, 2014). Baadhi ya tafiti zimebainisha kuwapo kwa changamoto ambazo zinatokana na matumizi ya mbinu hii katika ufundishaji na ujifunzaji LK. Mionganini mwa changamoto hizi ni kama; wajifunzaji kutopata faragha ya kutosha wakati wanapoishi na familia wenyeji, kuja kwa ndugu, rafiki na majirani katika familia zao bila taarifa na wajifunzaji kutopata chakula wanachokitarajia (Ngonyani, Mganga, Kisanji na Royer, 2016).

Licha ya tafiti hizo kubaini mchango na changamoto za matumizi ya mbinu hii, lakini hazikuchunguza ni kwa namna gani mbinu hii inaweza kuwa na mchango katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani. Hivyo basi, makala hii imechunguza mchango wa mbinu hii katika mchakato wa ufundashaji na ujifunzaji darasani wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Data za utafiti katika makala hii zimekusanywa kwa njia ya mahojiano kwa kuhusisha walimu 6 wa Kiswahili kwa wageni na wajifunzaji 6 wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Data zimekusanywa kutoka katika taasisi tatu; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Chuo cha Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa (MS TCDC)

Makala hii imegawika katika sehemu tatu kuu. Sehemu ya kwanza ni utangulizi wa jumla kuhusu makala haya, sehemu ya pili ni usuli kuhusu mkabala wa mawasiliano. Sehemu ya tatu ya makala inajadili mchango wa mbinu ya familia wenyeji katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani, na sehemu ya nne na ya mwisho ni hitimisho.

#### **Mkabala wa Mawasiliano**

Baada ya ufundishaji LK duniani kuititia historia ndefu na kufanya uboreshaji katika kila hatua, wanaisimu tumizi waliamua kuja na mikabala ya ufundishaji ambayo walifikiri ingekuwa suluhisho la changamoto ambazo zilikuwa zinatoka katika taaluma ya ufundishaji LK. Baadhi ya mikabala hiyo ni kama; mkabala wa sarufi tafsiri, mkabala wa moja kwa moja, mkabala wa mwitiko kwa vitendo tu, mkabala wa ujifunzaji kijumuiya, mkabala wa upendekezi, mkabala wa usikilizaji, mkabala wa utambuzi na mkabala wa mawasiliano. Katika mikabala hii, mkabala wa mawasiliano umesisitiza matumizi ya mbinu mbalimbali za ufundishaji wa lugha kwa kuzingatia mazingira halisi. Mbinu hizi ni kama vile; ziara za kimasomo, kualika mgeni darasani, rafiki wa lugha na familia wenyeji.

Mkabala wa mawasiliano ulitokana na nadharia ya lugha kama nyenzo ya kimawasiliano na lengo kuu la mkabala huu lilitokana na mtazamo wa Hymes (1972), uliotilia mkazo umahiri wa kimawasiliano katika ujifunzaji lugha na kutofautiana na Chomsky ambaye alidai kuijua lugha ni kuwa na umilisi wa kanuni za lugha inayohusika (Richards na Rodgers, 1986; Mtesigwa, 2009). Tafiti zilionesha kuwa wajifunzaji huweza kuwa mahiri kikanuni darasani lakini hushindwa kutumia lugha katika mawasiliano nje ya darasa na kuonesha kuwa umahiri wa kikanuni hautoshi katika ujifunzaji lugha (Larsen-Freeman, 2000). Mkabala wa mawasiliano ulipata umaarufu na kuingizwa katika mitaala ya ufundishaji LK kwa kuzingatia umahiri wa lugha inayohusika kuliko umahiri wa kanuni za lugha hiyo (Richards na Rodgers, 1986; Rasakumaran, 2019).

---

<sup>2</sup> Tafsiri ya ‘Homestay’. Hii ni mbinu ya kufundishia inayotumika katika programu za ujifunzaji lugha ng'ambo. Wajifunzaji huwekwa pamoja na familia zinazozungumza lugha husika kama wazawa na kuwa kama sehemu ya familia hizi ili waweze kujifunza lugha na utamaduni wa lugha husika.

Sifa kuu ya mkabala huu ni ufundishaji wa lugha kwa kuzingatia uwemo wa kuitumia lugha inayohusika katika mawasiliano (Larsen-Freeman, 2000). Ufundishaji lugha unaozingatia mkabala huu hujikita katika shughuli mbalimbali za darasani zenyenye kuweza kuibua mazungumzo kwa wajifunzaji, matumizi ya matini halisi na muktadha halisi wa ujifunzaji (Richards na Rodgers, 1989; Larsen-Freeman, 2000). Baadhi ya shughuli hizo ni kama ufanyakaji kazi katika vikundi, matumizi ya michezo ya lugha, maigizo dhima, shughuli za utatuza wa jambo fulani (Richards na Rodgers, 1989; Larsen-Freeman, 2000; Rasakumaran, 2019). Umahiri wa kiutamaduni pia ni kipengele muhimu kinachozingatiwa katika mkabala huu kwa kuwa utamaduni ni sehemu muhimu katika ujifunzaji lugha (Larsen-Freeman, 2000).

Katika kufanikisha umilisi wa kimawasiliano, mkabala huu umeonekana na watafiti wengi kuwa faafu ukilinganishwa na mikabala mingine ya kijadi. Mkabala huu umekuwa na matokeo chanya darasani kwa kuwa umemzingatia zaidi mijifunzaji hasa katika kipengele cha umilisi wa kuwasiliana kuliko umilisi wa kanuni za lugha (Larsen-Freeman, 2000; Makame, 2019). Katika ujifunzaji lugha kwa kuzingatia mkabala huu, ujifunzaji LK katika muktadha halisi umesisitizwa zaidi. Ujifunzaji huu huhusisha mbinu mbalimbali na mionganoni mwa mbinu hizi ni kwenda katika ziara za kimasomo, kualika mgeni darasani, wajifunzaji kukutanishwa na wazungumzaji wazawa na kuwa kama rafiki zao wa lugha na kuishi na familia wenyeji. Makala hii imeshughulikia mbinu ya familia wenyeji kama mbinu inayopendekezwa na mkabala wa mawasiliano.

### **Mbinu ya Kuishi na Familia Wenyeji**

Wajifunzaji wanaokwenda ng'ambo kujifunza lugha hutarajiwa kupata fursa kubwa ya kuwasiliana katika miktadha halisi ya mazungumzo kwa kuwa kwa kiasi kikubwa huchangamana na wazawa wa lugha hiyo. Moja ya fursa ya kuchangamana na wazungumzaji wazawa wa lugha inayohusika ni kukaa ndani ya familia wenyeji (Rivers, 1998; Wilkinson 1998; Wilkinso 2002; Macheno, 2008). Familia wenyeji ni mbinu ambayo hutumika katika programu za ujifunzaji lugha ng'ambo ambapo wajifunzaji hupewa fursa ya kuishi pamoja na wazungumza lugha wazawa katika lugha inayohusika. Ife (2000) katika Juveland (2011:3) anaelezea kuwa, moja kati ya motisha kubwa ya kujifunza lugha ng'ambo ni fursa ya kuitumia lugha husika nje ya mazingira ya darasa.

Tafiti nyingi zimeonesha kuwa matumizi ya mbinu hii yameleta tija kwa wajifunzaji kwa kukuza viwango vyao vya lugha katika ujifunzaji LK (Archangeli, 1999). Naye Macheno, (2008) anashadidia hoja hii kuwa wajifunzaji wanaoshiriki katika programu za ujifunzaji lugha ng'ambo wanapiga hatua kubwa katika ujifunzaji ikilinganishwa na wajifunzaji wanaojifunza katika nchi zao (Macheno, 2008). Wajifunzaji wa LK wanaojifunza lugha ng'ambo huwa na fursa kubwa ya kuitumia lugha katika mazingira yasiyotabirika kwa kuwa wanapojifunza darasani huweza kujua nini kimepangwa kujifunza katika siku husika au kipindi husika cha kozi. Kwa mujibu wa Macheno, (2008) wajifunzaji hukuza viwango vyao vya kujifunza lugha wanapojifunza LK ng'ambo, lakini aina ya makazi huweza kuchangia pia. Wajifunzaji wanaoishi na familia wenyeji wanaonekana kuwa na maendeleo zaidi katika ujifunzaji ikilinganishwa na wanaoishi mabwenini au katika aina nyingine ya makazi. Tafiti tangulizi kama vile; Crealock, Derwing na Gibson, (1999), Naye Barron, (2003), Freed, Segalowitz, Lafford na Diaz-Campos (2004), Gutel, (2008), Juveland, (2011) na Naye Parry, (2014) zimejikita katika kuchunguza mchango wa kutumia mbinu hii katika maendeleo ya LK kwa wajifunzaji bila kuangalia ni kwa namna gani maendeleo haya yanaweza kuwa na mchango katika ufindishaji na ujifunzaji darasani.

Katika muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya kigeni, Ngonyani, Mganga, Kisanji na Royer, (2016) walichunguza hatua za mabadiliko ya mtazamo wa utamaduni kwa wajifunzaji wa programu ya Mradi wa Idara ya Elimu (GPA - Fulbright - Hayes) ambao unafadhiliwa na serikali ya Marekani. Utafiti huu ulichunguza ni kwa namna gani wajifunzaji wa Kiswahili wanaokuja nchini Tanzania na kukaa na familia wenyeji wanapitia mabadiliko ya utamaduni kama ilivyoelezwa na Hamer (2011) na Bennet (1993). Mabadiliko haya ya mtazamo wa utamaduni ambayo yameelezw na Hamer na Bennet ni; (i) kuukataa utamaduni mpya, (ii) kujihami katika utamaduni wake, (iii) kupuuzia tofauti zinazojiteza, (iv) kuukubali utamaduni mpya. (v) kujirekebisha na kuendana na utamaduni mpya, na (vi) kujichanganya katika utamaduni huo.

Utafiti huu ulijikita katika kuangalia uzoefu wa uendeshaji programu hii na kutazama changamoto ambazo wajifunzaji walikabiliana nazo katika kuzoea utamaduni wa wenyeji wakati wa kukaa pamoja na familia wenyeji. Utafiti ulichunguza ni kwa namna gani wajifunzaji walivyokuja na kumaliza mafunzo yao. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwapo kwa changamoto nyingi za migongano ya kiutamaduni kati ya wajifunzaji na familia wenyeji zilizosababishwa na kutofanyika kwa maandalizi ya kutosha kabla ya wajifunzaji kwenda kukaa na familia wenyeji.

Licha ya kuwa utafiti huu umeshughulikia familia wenyeji, haukutazama familia wenyeji kama mbinu ya ufundishaji LK, umechunguza tu mabadiliko ya kimtazamo katika kuzoea utamaduni mpya. Kwa kuwa wajifunzaji hawa walikuja kwa ajili ya kujifunza Kiswahili kama LK na imedhihirika kuwepo kwa changamoto za migongano ya kiutamaduni kati ya wajifunzaji. Makala hii imechunguza mchango wa mbinu ya familia wenyeji katika ufundishaji na ujifunzaji darasani wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa wajifunzaji wanaokuja nchini Tanzania.

#### **Nadharia ya Umahiri wa Kimawasiliano na Tamaduni Mchanganyiko**

Nadharia ya Umahiri wa Kimawasiliano na Tamaduni Mchanganyiko<sup>3</sup> iliasisiwa na Hall (1992). Nadharia hii ilitokana na mawazo ya awali ya Hall (1956) katika kitabu chake cha *The Silent Language*. Hoja kuu ya nadharia hii ni kuwa na umahiri wa kimawasiliano na utamaduni huchangiwa zaidi na mjifunzaji kuchangamana na wenyeji wa utamaduni unaohusika. Kwa Hall ili mjifunzaji aweze kuwa mahiri katika kipengele cha mawasiliano na utamaduni ni lazima aelewe tofauti kati ya utamaduni wake na wa lugha anayojifunza, aelewe miiko, mila na desturi za watu wa lugha anayojifunza.

Hall (1992) anafafanua kuwa uwezo wa kuitumia lugha kwa kujua kanuni zake na kuwa na umilisi wa stadi zote ni jambo muhimu, ila ni muhimu zaidi kwa mjifunzaji wa LK kujua namna ya kuwasiliana na watu hao kwa kujua masuala muhimu ya utamaduni wa wazungumzaji wa lugha hiyo. Kwa kuwa ujifunzaji wa lugha ya kigeni humtaka mjifunzaji kuchangamana na watu wa tamaduni zingine, Hall anasisitiza suala la umahiri wa kimawasiliano na utamaduni ili kuweza kuwa mahiri katika lugha. Mjifunzaji anaweza kuwa mahiri katika mawasiliano lakini akaukosa muktadha kimawasiliano kwa kuukosa umahiri wa tamaduni mchanganyiko kama vile kujua tabia mbalimbali za kitamaduni ambazo zinaambatana na matumizi ya lugha (Yu, 2020).

Mbinu ya familia wenyeji ni mbinu ambayo inampa fursa mjifunzaji kuchangama na familia ambayo inazungumza lugha ya kigeni anayojifunza mjifunzaji kama wazawa wa lugha hiyo. Fantini, (2018) anafafanua kuwa kukaa na familia wenyeji ni muhimu sana kwa mjifunzaji anayeshiriki programu ya ujifunzaji lugha ng'ambo kwa kuwa mjifunzaji huyu hupata fursa ya kukuza na kuendeleza umilisi wake wa lugha ya kigeni. Mjifunzaji huyu hutarajiwa kukuza na kuendeleza umahiri wake wa lugha ya kigeni kwa kuwa kukaa na familia wenyeji kunampa nafasi ya kuwa mahiri wa kimawasiliano na kuchangamana na watu wenye utamaduni wa LK inayohusika. Mbinu ya familia wenyeji imesisitizwa sana na mkabala huu wa kinadharia.

Msingi ya nadharia hii ni; motisha ya kujifunza lugha na utamaduni unaohusika, maarifa kuhusu lugha na utamaduni unaohusika wakati wa ujifunzaji lugha ya kigeni na stadi za kuweza kukabiliana na tofauti kati ya tamaduni mbili tofauti wakati wa kujifunza lugha ya kigeni na kuchangamana na wazawa wa lugha inayohusika.

**Mchango wa Mbinu ya Familia Wenyeji katika Mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji Darasani** Watoa taarifa walioshiriki katika kutoa taarifa zilizofanikisha makala hii, walieleza kuwepo mchango katika kutumia mbinu hii katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani. Washiriki hawa walikuwa walimu wa Kiswahili kama lugha ya kigeni 9, wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni 9 na waratibu wa familia wenyeji 3. Watoa taarifa walibainisha mchango wa mbinu ya familia wenyeji katika ufundishaji na ujifunzaji darasani wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kama ifuatavyo.

---

<sup>3</sup> Tafsiri ya ‘Intercultural Communicative Competence (ICC)’

### Kukuza Kiwango cha Msamiati

Alqahtani, (2015) anaeleza kuwa msamiati ni jambo la msingi katika kujifunza lugha ya kigeni kwa kuwa ndio msingi mkuu wa mjifunzaji kujifunza lugha ya kigeni inayohusika. Ili mjifunzaji aweze kutumia lugha vizuri na kuweza kuwasiliana na watumiaji wa lugha hiyo, hana budi kukuza kiwango chake cha msamiati. Kiwango cha msamiati huwasaidia wajifunzaji kuimairisha stadi zote za ujifunzaji lugha ya kigeni. Mjifunzaji huweza kuimairisha stadi ya kusikiliza kwa kuwa ataaelewa mazungumzo kutohana na kuwa na uelewa mpana wa msamiati. Vilevile, atakuza stadi ya kuzungumza, kuandika na kusoma pia. Nadharia ya umahiri wa kimawasiliano na tamaduni mchanganyiko inasisitiza kuwa mjifuzaji wa lugha ya kigeni ahimizwe kuchangamana na wazungumzaji lugha wazawa wa lugha ya kigeni inayohusika ili kukuza kiwango chao cha msamiati na kusabibisha kupiga hatua kimaendelo katika ujifunzaji wao wa lugha.

Walimu 9, wajifunzaji 8 na waratibu 2 ambao walishiriki katika mahojiano walieleza kuwa wajifunzaji wanapokaa na familia wenyeji huwasaidia mno kukuza viwango vyao vya msamiati. Msamiati huu huwasaidia sana darasani wakati wa kujifunza pamoja na walimu wao. Wajifunzaji hawa huja na maneno mapya mengi ambayo wameyapata kutoka katika familia zao na maneno haya huwa sehemu ya mjadala darasani. Walimu walieleza kuwa asubuhi kabla ya kutambulisha somo la siku huwa na mjadala wa maneno mapya ambayo wameyapata kutoka katika familia wenyeji.

Licha ya kuonekana kuwa ni mbinu inayomsaidia mjifunzaji kujifunza utamaduni na kukuza kiwango cha lugha nje ya darasani kama ilivyobainishwa na; (Macheno, 2008; Juveland, 2011 na Ngonyani, Mganga, Kisanji na Royer, 2016), mbinu hii inaonesha wazi kuwa na mchango wa moja kwa moja katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni darasani kama ilivyobainishwa na watoa taarifa katika makala hii.

### Kuchochea Mazungumzo Darasani

Mazungumzo ni jambo muhimu kwa mjifunzaji anayejifunza lugha ya kigeni. Donaldson, (2011) anaeleza kuwa mjifunzaji wa lugha ya kigeni hana budi kujihusisha katika mazungumzo ili kukuza stadi yake ya kusikiliza na kuzungumza. Stadi hizi ni stadi za awali na msingi katika kujifunza lugha ya kigeni. Ili mjifunzaji aweze kujihusisha katika mazungumzo, ni lazima pawepo na motisha ya kumfanya mjifunzaji huyo avutiwe na mazungumzo. Macheno, (2008) anaeleza kuwa wajifunzaji wa lugha ya kigeni huvutiwa na mazungumzo ambayo huwasaidia si tu kukuza maarifa yao ya kujifunza lugha ya kigeni inayohusika, lakini pia kuwaonzeza maarifa kuhusu utamaduni na masuala mbalimbali mtambuka yanayahuju jamii hiyo. Wajifunzaji wanapokaa na familia wenyeji hupata fursa hii kwa kuwa hujifunza mambo mbalimbali mtambuka ambayo hukuzma maarifa yao ya lugha ya kigeni na kukuza maarifa yao lugha inayohusika wanayojifunza (Juveland, 2011).

Katika mahojiano walimu 4, wajifunzaji 5 na waratibu 2 walieleza kuwa wajifunzaji wanapokaa na familia wenyeji hujihusisha katika mazungumzo huru na wanafamilia. Mazungumzo haya mara nyinyi huwa ni yale ambayo hayana mipaka maalumu<sup>4</sup> kama yale ya darasani. Wajifunzaji wanapokuja darasani huja na mada mbalimbali ambazo wamezungumza nyumbani na wanafamilia na kuibua mjadala. Mijadala hii hupendeleva na wajifunzaji kwa kuwa inawapa uhuru wa kuzungumza zaidi ya kile kilichoandaliwa darasani na kuwafanya kuongeza maarifa ya nchi, utamaduni na mambo mtambuka yanayojiri nchini. Wajifuzaji huwa na shauku ya kuja darasani na kuzungumza mambo ya nyumbani tofauti na anayetokea bwenini.

Katika mahojiano mwalimu mmoja alieleza kuwa wajifunzaji wanaokaa katika familia wenyeji huweza kushiriki katika mazungumzo darasani kwa kuzungumza na kutumia miundo mbalimbali yenye kuwasilisha dhana moja. Mwalimu alitoa mfano wa mjifunzaji kusema “nina njaa/chakula tayari?/tunakula saa ngapi?”. Miundo hii huwa ni nadra sana kutumiwa darasani na wajifunzaji wanakaa mabwenini.

<sup>4</sup> *Unstructured conversation*, Haya ni mazungumzo ya kawaida ambayo hayana mipaka na wazungumzaji wake hawajandai. Aina hii ya mazungumzo ni tofauti na yale ya darasani ambayo hujikita katika mada fulani ya somo la siku husika. Wajifunzaji hujikita kuzungumza katika mada inayohusika tu.

Nadharia ya umahiri wa kimawasiliano na tamaduni mchanganyiko ya Hall, (1992) inasisitiza mjifunzaji kujihusisha katika mazungumzo ili kutanua maarifa kuhusu lugha na utamaduni wa lugha ya kigeni anayojifunza. Pamoja na mbinu hii ya familia wenyeji kuwa na mchango kwa wajifunzaji katika kukuza viwango vyao lugha kupitia mazungumzo na familia wenyeji kama ilivyobainishwa na; (Barron, 2003; Freed, Segalowitz, Lafford na Diaz-Campos 2004; Gutel, 2008 na Juveland, 2011), mbinu hii pia ilionekana kuwa na mchango katika ufundishaji na ujifunzaji darasani.

#### **Kukuza Stadi ya Kusikiliza na Kuzungumza**

Stadi ya kusikiliza na kuzungumza zimetiliwa mkazo na watafiti wengi kuwa ni stadi za msingi katika kujifunza lugha ya kigeni (Jayaraman, 2011). Wajifunzaji lugha huanza na stadi ya kusikiliza kwa kuwa huanza kusikia lugha kisha kujifunza kuzungumza lugha hiyo. Watoa taarifa walieleza katika mahojiano kuwa wajifunzaji ambao wanakaa katika familia wenyeji huwa na muda mwangi wa kufanya mazoezi ya kuzungumza na kusikiliza wanafamilia wanapokuwa nyumbani. Fursa hii ya kufanya mazoezi ya kuzungumza na wanafamilia wakiwa nyumbani huwasaidia kukuza stadi zao za kuzungumza na kusikiliza. Kukua kwa stadi ya kusikiliza na kuzungumza huwa na mchango mkubwa darasani kwa wajifunzaji. Wajifunzaji huweza kushiriki vyema darasani kwa kuchangia mijadala.

Walimu 5 ambao walishiriki katika mahojiano walieleza kuwa wajifunzaji waliokaa katika familia wenyeji waliweza kufanya vizuri zaidi katika mitihani yao kupima umahiri wa kuzungumza Kiswahili. Darancik, (2018) anaeleza kuwa ili mjifunzaji wa lugha ya kigeni aweze kuwa mahiri katika lugha hana budi kuimarisha stadi ya kuzungumza kwa kuwa ndio stadi ya msingi katika ujifunzaji. Hall, (1992) katika nadharia ya umahiri wa kimawasiliano na tamaduni mchanganyiko anasisitiza kuwa mjifunzaji hana budi kuchangamana na wazawa wa lugha ya kigeni anayojifunza ili kuimarisha stadi zake za kusikiliza na kuzungumza na kuweza kuwasiliana vizuri kwa kuzingatia pia kanuni za kiutamaduni katika mawasiliano.

#### **Kuongezeka kwa Kiwango cha Kujihamini wakati wa Kutumia Lugha**

Kujihamini ni suala la msingi katika kujifunza lugha ya kigeni. Gabejan, (2021) anafafanua kuwa wajifunzaji wanaweza kufanya vizuri zaidi katika kuendeleza stadi zao za lugha iwapo wataondolewa wasiwasi na kujengewa uwezo wa kujihamini katika kutumia lugha ya kigeni wanayojifunza. Zeng na Cheng, (2018) wanaeleza kuwa kufahamu sababu za wasiwasi wa wajifunzaji katika kujifunza lugha ya kigeni husaidia kuwaondolea wajifunzaji wasiwasi huo na kuweza kufanikisha ujifunzaji kwa urahisi. Wajifunzaji wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni huwa na wasiwasi huo pia katika kutumia lugha wakati wanajifunza. Walimu na waratibu ambao wameshiriki katika mahojiano walieleza kuwa wajifunzaji wa Kiswahili ambao wanakuja kujifunza, wanakuwa na wasiwasi wa kutumia lugha kwa hofu ya kuchekwa au kuonekana hawana bidii katika kujifunza. Wale ambao hukaa na familia wenyeji huondoa wasiwasi huu wa kutumia lugha kwa sababu ya kuchangamana na wanafamilia katika familia zao. Hali hii huleta mchango darasani kwa kuwa wajifunzaji hawa huondoa wasiwasi huu wa kutumia lugha darasani na kusababisha kupiga hatua katika viwango vyao vya lugha.

#### **Kuondoa kwa Hofu ya Kufanya Makosa ya Kisarufi**

Kwa mujibu wa Wood, (2017) makosa ya kisarufi ni jambo ambalo hufanywa kwa kawaida na wajifunzaji wa lugha ya kigeni kutokana na sababu mbalimbali. Athari za lugha ya kwanza/mama ya mzungumzaji na wasiwasi ni mambo makuu ambayo huweza kusababisha makosa haya. Wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni pia hufanya makosa ya kisarufi kama ilivyobainishwa na tafiti mbalimbali kama vile Simba, (2014) na Mkomwa, (2019). Walimu 5 walioshiriki mahojiano walieleza kuwa wajifunzaji ambao huwfundisha hufanya makosa ya kisarufi na sababu kuu huwa ni hofu ya kufanya makosa ya kisarufi. Baada ya kukaa katika familia wenyeji kwa muda, wajifunzaji huonekana kuondoa hofu hiyo ya kufanya makosa ya kisarufi kwa kuwa wanatumia zaidi Kiswahili katika mazingira ambayo wanakuwa huru.

Hali hii ya kuondoa hofu wakiwa na familia wenyeji huhamia darasani na kusaidia wajifunzaji kutokuwa na hofu ya kufanya makosa ya kisarufi darasani na kuzingatia zaidi mawasiliano. Walimu

walieleza katika mahojiano kuwa hofu ya kufanya makosa ya kisarufi ikiondoka, wajifunzaji huweza kupiga hatua zaidi katika ujifunzaji. Courtad na Courtad, (2019) wanaeleza kuwa wajifunzaji huhitaji zaidi kuondolewa hofu ya kufanya makosa ya kisarufi ili ufundishaji na ujifunzaji uwe na tija. Wajifunzaji wanaoondolewa hofu hii huweza kuwa mahiri katika lugha ya kigeni wanayojifunza. Hii inaonesha wazi ni kwa namna gani mbinu ya familia wenyeji inaweza kuwa na mchango katika ufundishaji na ujifunzaji darasani wa Kiswahili kama lugha ya kigeni.

### **Hitimisho**

Mbinu ya familia wenyeji ni mbinu ya ujifunzaji lugha kindakindaki iliyopendekezwa na mkabala wa mawasiliano. Mbinu hii inatumiwa na walimu wanaofundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni nchini Tanzania. Tafiti zilizofanyika zimeweza kuonesha ni kwa namna gani mbinu hii ina mchango katika ujifunzaji wa jumla wa lugha ya kigeni. Makala hii imebainisha mchango wa mbinu hii katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni darasani. Mbinu hii ya familia wenyeji imeonekana kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na mchakato wa ujifunzaji wa darasani. Tafiti zilizofanyika zimeinbainisha mbinu hii kama mbinu ambayo inajitegemea na hazikuonesha uhusiano huu uliopo kati ya mbinu hii ya kukaa na familia wenyeji na mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani.

### **Marejleo**

- Alqahtani, M. (2015). The Importance of Vocabulary in Language Learning and How to be Taught. *International Journal of Teaching and Education*. Juz. 3(3): 21-34
- Archangeli, M. (1999). Study Abroad and Experiential Learning in Salzburg, Austria. *Foreign Language Annals*. Juz. 32(1): 155-122
- Barron, A. (2003). *Acquisition in Interlanguage Pragmatics: Learning How to do Things with Words in a Study Abroad Context*. Amsterdam: John Benjamins.
- Bennet, M.J. (1986). A development Approach to Training for Intercultural Sensitivity. *Intercultural Journal of Intercultural Relations*. Juz. 10: 179 - 196.
- Courtad, C. C na Courtad, C.A (2019). The Use of English Grammar and Confidence Level of the Student when Writing in Spanish. *Journal for Research and Practice in College Teaching*. Juz. 4(1): 170-188.
- Crealock, E., Derwing.T. M., na Gibson, M. (1999). To Homestay or to Stay Home: The Canadian-Japanese Experience. *TESL Canada Journal*. Juz. 16(2): 53-61.  
Inapatikana katika <https://files.eric.ed.gov/fulltext/EJ585974.pdf>
- Darancik, Y. (2018). Students' Views on Language Skills in Foreign Language Teaching. *International Education Studies*. Juz. 11(7): 166-178.
- Di Silvio, F., Donovan, A. na Malone, M.E. (2014). The Effect of Study Abroad Homestay Placements: Participant, Perspective and Oral Proficiency Gain. *Foreign Langauge Annals*. Juz 47: 169-188.
- Donaldson, R. M. (2011). *Teaching Foreign Language Converstaion: A Conversation Norms Approach*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Jimbo la Carlifonia, Chiko.
- Freed, B.F., Segalowitz, N. na Dewey, D. P. (2004). Context of Learning and Second Language Fluency in French – Comparing Regular Classroom, Study Abroad and Intensive Domestic Immersion Programs. *Studies in Second Language Acquisition*. Juz. 26(2): 275-301.
- Gabejan, A. M. C.(2021). Enhancing Students' Confidence in an English Language Classroom. *International Journal of English Language Studies*. Juz. 3(5):16-25.
- Gutel, H. (2008). The Homestay: A Gendered Perspective. *Frontiers: The Interdisciplinary Journal of Study Abroad*. Juz. 1: 173-188. Inapatikana katika <https://files.eric.ed.gov/fulltext/EJ878389.pdf>
- Hymes, D. (1972). 'On Communicative Competence'. Katika Pride, J na Holmes, J (wah). *Social Linguistics: Selected Readings*. Harmondsworth: Penguin Books: 269-293.
- Isabelli, C. (2000). *Motivation and Extended Interaction in the Study Abroad Context: Factors in the Development of Spanish Language Accuracy and Communication Skills*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Texas cha Austin.
- Jayaraman, S. (2011). Focus on Listening for Developing Speaking Skills in Learning a Second Language. *CONFLUENCE*. Juz 1: 59-66.

- Juveland, S. R. (2011). *Foreign Language Students' Beliefs about Homestays*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Portland.
- Larsen-Freeman, D. (2000). *Techniques and Principles of Language Teaching*. (Toleo la 2). Oxford. Oxford University Press.
- Macheno, A. A. (2008). *A Study of Effect of Study Abroad and Homestay on the Development of Linguistic and Interactional Practices by Spanish L2 Learners*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Texas at Austin.
- Makame, K. O. (2019). Mkabala wa Kimawasiliano katika Ufundishaji wa Lugha ya Pili: Mifano kutoka Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni Tanzania. *Kiswahili, Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*. Juz. 82: 72-85.
- Mkomwa, G. (2019). *Dosari za Kimofosintaksia Zinazofanywa na Ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa Lugha ya Kigeni*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.
- Mtesigwa, P. C. K. (2009). Utayarishaji wa Vitabu vya Kufundishia Kiswahili kama Lugha ya Kigeni: Haja ya Kuzingatia Mkabala wa Kimawasiliano. *Kiswahili, Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Juz. 72 : 52-67.
- Ngonyani, D, Mganga, Y, Kisanji, J na Royer, O. (2017). Maendeleo ya Wanafunzi katika Kujifunza Utamaduni Mpya Ng'ambo katika Familia: Uzoefu wa Mradi wa GPA Kiswahili. *Journal of African Language Teachers Association*. Juz. 3: 1-24.
- Parry, M. (2014). *Australian University Students and their Japanese Host Families in Short-term Homestays: Perceptions, Intercultural Issues and Relational Dynamics*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Queensland.
- Rasakumaran, A. (2019). A Brief History of Foreign Langauge Teaching. *Language in India*. Juz. 19(5): 93-106.
- Richards, J. C. na Rodgers, T. S. (1986). *Approches and Methods in Language Teaching: A Discription Analysis*. Cambridge. Cambridge University Press.
- Rivers, W. P. (1998). Is Being there Enough?: The Effects of Homestay Placements on Language Gain During Study Abroad. *Foreign Language Annals*. Juz. 31(4): 492-500.
- Simba, E. (2014). *Matatizo ya Kisarufi katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Pili kwa Wageni*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Wood, J. F. (2017). Errors in Second/Foreign Language Learning and Their Interpretation. *Education and Linguistics Research*. Juz. 3(1): 1-14.
- Wilkinson, S. (1998). Study Abroad from the Participants' Perspective: A Challenge to Common Beliefs. *Foreign Language Annals*. Juz. 31: 23-40.
- Wilkison, S. (2002). The Omnipresent Classroom During Summer Study Abroad: American Students in Conversation with their French Hosts. *The Modern Language Journal*. Juz. 86:157-173.
- Zeng, Y. na Cheng, L. (2018). How Does Enxiety Influence Language Performance? From the Perspectives of Foreign Language Classroom Anxiety and Cognitive Test Anxiety. *Language Testing in Asia*. Juz. 8(13): 1-19.